**HOTUBA YA MHESHIMIWA SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KWENYE MKUTANO NA WANAWAKE DODOMA, TAREHE 8 JUNI, 2021**

*Mheshimiwa Dorothy Gwajima, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto;*

*Waheshimiwa Wenza wa Viongozi mliopo;*

*Waheshimiwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano pamoja na Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi;*

*Waheshimiwa Mawaziri wengine mliopo;*

*Mheshimiwa Gaudensia Kabaka, Mwenyekiti wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT);*

*Mheshimiwa Anthony Mtaka, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma;*

***Ndugu Makatibu Wakuu pamoja na Viongozi wengine wa Serikali mliopo;***

***Viongozi wetu wa Dini na Vyama na Siasa mliopo;***

***Ndugu Wanawake Wenzangu, Wageni Waalikwa wote;***

***Wasanii, Wanafunzi, Wana-Habari, Mabibi na Mabwana;***

**NAWASALIMU KWA JINA LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

Awali ya yote, namshukuru sana Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, kwa kutujalia uhai na kutuwezesha kukutana hapa leo tukiwa wenye afya njema. Aidha, nawashukuru Viongozi wa Wizara ya Afya, Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT), Mkoa wa Dodoma pamoja na wote walioshirikiana nao kwenye maandalizi ya Mkutano

huu. Nafahamu muda ulikuwa mfupi, na kusema kweli sikutegemea kama watu wangekuwa wengi namna hii. Hivyo, hongereni na ahsanteni sana.

Nawashukuru pia wanawake wote mliojitokeza kwa wingi kwenye Mkutano huu. Nafahamu, baadhi yenu mmetoka mbali, nje ya hapa Dodoma mjini, na kama tulivyosikia, wapo walitoka Zanzibar. Natambua pia wapo wanawake wengine wengi wanaofuatilia Mkutano huu kwa njia ya luninga na mitandao ya kijamii. Wote nawashukuru. Shukrani zetu za dhati ni kwa wanaume waliopo hapa ukumbini na wale wanaotufuatilia kupitia vyombo mbalimbali. Hakika inafurahisha kuungwa mkono nanyi. Tunawashukuru sana.

Kabla sijaendelea zaidi, kama mnavyofahamu, leo ni mara yangu ya kwanza kuzungumza na wanawake tangu nimekabidhiwa kijiti cha kuliongoza Taifa letu. Hivyo basi, napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani nyingi na za dhati kwa wanawake wote wa Tanzania kwa kuonesha imani na kumchagua kwa kura nyingi kwenye Uchaguzi Mkuu uliopita, Hayati Dkt. John Pombe Magufuli kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mimi kuwa Makamu wa Rais. Maamuzi yenu yale ndiyo yaliyonifanya mimi kuwa hapa, baada ya kudra ya Mwenyezi Mungu ya kumwita kwake mpendwa wetu, Hayati Rais Dkt. Magufuli. Na kutokana na ukubwa wa Mkutano huu, naomba sote tusimame kwa dakika moja, kumkumbuka na kumwombea. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. Amina.

Kwa namna ya pekee, nakishukuru Chama changu Cha Mapinduzi (CCM), ambacho kilikubali kwa mara ya kwanza kupendekeza jina la mwanamke kuwa Mgombea Mwenza kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015; na pia kwenye Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Uwepo wangu hapa leo unatokana na matakwa ya Katiba yetu, ambayo inaelekeza kuwa endapo Rais aliyopo madarakani atashindwa kuendelea na majukumu hayo kwa sababu yoyote, Makamu wa Rais atachukua jukumu hilo. Kwa msingi huo, napenda kurudia kukishukuru Chama changu lakini pia wanawake na Watanzania wote kwa ushirikiano mkubwa mnaonipa tangu nimepata dhamana ya kuliongoza Taifa letu. Ahsanteni sana.

*Ndugu Wanawake na Watanzania Mnaonisikiliza;*

Nimekuja kuzungumza na wanawake wa Dodoma, kwa niaba ya wanawake wote wa Tanzania, ili kuendeleza utaratibu niliojiwekea wa kukutana na makundi mbalimbali kwa makusudi ya kubadilishana mawazo na kusikia kutoka kwao vile wangependa nchi yetu iongozwe. Mtakumbuka kuwa, mpaka sasa, tayari nimekutana na Viongozi wa Dini hapa Dodoma, Wazee pale Dar es Salaam, na pia Viongozi wa Taasisi ya Sekta Binafsi; na siku chache zijazo nitazungumza na vijana kule Mwanza.

Leo ni zamu ya wanawake. Na katika hilo, napenda nitamke, hapa mwanzoni kabisa kuwa, nimefurahishwa sana na kaulimbiu ya Mkutano huu inayosema **"Mwanamke ni Nguzo ya Maendeleo: Tujitambue,**

**Tujidhatiti, Tutekeleze Wajibu wetu"**. Kwa hakika, wanawake ni chachu ya maendeleo kwenye Taifa lolote. Hakuna Taifa linaloweza kupiga hatua za kimaendeleo bila ya kuwategemea wanawake.

Na hii ni kwa sababu kubwa mbili. Ya kwanza ameieleza vizuri msoma Risala, kwamba wanawake ni jeshi kubwa. Wanawake tupo wengi sio tu hapa nchini bali duniani kote. Kwa hapa nchini, takwimu zinaonesha kuwa wanawake tupo **asilimia 51.04**. *Lakini, kama hiyo haitoshi, nyote mnafahamu kuwa, wanawake ndiyo wameileta duniani asilimia nyingine inayobaki*. Hii inadhihirisha kuwa wanawake ni kundi kubwa na hivyo hatupaswi kuwa wanyonge.

Lakini ukiachilia mbali idadi, wanawake wanatoa mchango mkubwa kwenye shughuli za kimaendeleo. Mathalan, sote tunafahamu mchango mkubwa uliotolewa na wanawake wakati wa harakati za ukombozi wa Taifa letu na pia baada ya kupata Uhuru. Kuna usemi unasema, *"ukienda kuvuna ujue kuna watu walikata msitu, wakalima, wakapanda, wakapalilia, wakavuna mazao mpaka ikafika wakati wa mavuno"*. Hii ina maana kuwa sisi tuliopo hapa leo, tunavuna matunda au mazao ambayo wanawake wengi wa zamani waliyatayarisha (bibi zetu, mama zetu na dada zetu). Hivyo basi, hatuna budi kuwashukuru wote waliotutangulia na leo tunafaidi matunda yao. Na kwa wale waliotangulia mbele za haki, tuzidi kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu.

***Ndugu zangu Wanawake;***

Nchi yetu imetunga Sera na Sheria pamoja na kuridhia na kutekeleza Mikataba na Maazimio mbalimbali ya Kikanda na Kimataifa, ikiwemo Mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Kutokomeza aina zote za Ubaguzi dhidi ya Wanawake (1979), Azimio la Beijing la mwaka 1995; Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Mtoto (1989); Malengo ya Maendeleo Endelevu (2030); na Ajenda ya Maendeleo ya Afrika tuitakayo (2063). Kutokana na utekelezaji wa Sheria na maazimio hayo, tumeweza kupata mafanikio mengi makubwa kama ifuatavyo:

*Mosi, Uwiano wa Jinsia katika vyombo vya Maamuzi na Ajira*: Sio siri kuwa mafanikio makubwa yamepatikana katika eneo hili. Na mfano halisi ni mimi mwenyewe. Kwenye

miaka thelathini au ishirini iliyopita, jambo hili halikufikirika; lakini mwaka 2015, nchi yetu iliingia kwenye historia ya kumpata mwanamke wa kwanza kuwa Makamu wa Rais na sasa tunaye Rais mwanamke. Lakini mbali na hilo, idadi ya wanawake kwenye vyombo vingine vya maamuzi nayo imeongezeka ikiwemo Mabaraza yetu ya Mawaziri, Wakuu wa Mikoa, Makatibu Wakuu, n.k. Hivi karibuni tumeteua Makatibu Tawala **26** ambapo wanawake walikuwa **12**; sawa na **asilimia 46**.

Kwa upande wa Mahakama, mtakumbuka pia kuwa, mwezi uliopita, tuliteua Majaji **28**, ambapo **12** ni wanawake, sawa na takriban **asilimia 43**. Hii imeongeza idadi ya majaji wanawake hadi kufikia **29** kati ya Majaji **86** waliopo, ambao ni sawa na takriban **asilimia 34**. Bungeni nako, kwa kipindi

cha pili sasa, tumekuwa na Naibu Spika ni mwanamke, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson. Aidha, idadi ya Wabunge wanawake nayo imeongezeka kutoka wabunge **127** mwaka 2015 hadi kufikia **143** mwaka 2020; na kwa mara ya kwanza kwenye historia ya nchi yetu, nimemteua Katibu wa Bunge mwanamke. Hii inanipa matumaini kuwa, kwenye miaka michache ijayo, tutafikia usawa wa kijinsia kwenye vyombo vya maamuzi.

Lakini, pamoja na mafanikio yaliyopatikana kwenye eneo la vyombo vya maamuzi, kwa sasa, changamoto kubwa ni kwamba, wanawake wengi hawapo kwenye ajira rasmi. Takriban **asilimia 70** ya wanawake wapo kwenye ajira isiyo rasmi, biashara ndogo ndogo, migodini, kazi za majumbani, n.k. Kwa mfano, kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2017,

kati ya watu **3,014,106** waliokuwa kwenye ajira rasmi, wanawake walikuwa **1,107,917** sawa na **asilimia 36.8** tu.

Hali hii inasababishwa na mambo mengi, mojawapo ikiwa wanawake kukabiliwa na majukumu mengi ya kifamilia; na hivyo kufanya waajiri, hususan wa sekta binafsi, kutopenda sana kuwaajiri wanawake**.** Sababu ya pili ni ukosefu wa ujuzi. Hata hivyo, napenda kutumia fursa hii kuipongeza Sekta yetu Binafsi, ambayo baada ya kufanya utafiti ambao ulionesha kuwa kampuni zenye idadi kubwa ya wanawake zinapata faida zaidi ukilinganisha na zenye idadi ndogo, waliamua kuandaa mkakati maalum wa kuanzisha mafunzo ya kuwapatia ujuzi wanawake yatakayowawezesha kuajirika na kupewa majukumu makubwa kwenye mashirika. Hivyo, narudia

kuipongeza sekta yetu binafsi na naiomba iridhie kuendelea kuchangia tozo ya kukuza ujuzi (*skills development levy*) ambayo inatusaidia kujenga vyuo vya ufundi. Kwa upande wetu Serikali, tutaendelea kuongeza fursa za ajira kwa wanawake, kwa kadri inavyowezekana.

***Wapendwa Wanawake wenzangu;***

Ukiachilia mbali eneo la uongozi na ajira, hatua kubwa imepigwa katika kuelekea uwiano wa kijinsia kwenye eneo la Elimu, ambapo kwa sasa uwiano kati ya wavulana/wanaume na wasichana/wanawake kuanzia shule za msingi hadi vyuo vikuu unakaribiana. Kwa mfano, Shule za Msingi zina wanafunzi **milioni 11.2**, ambapo wasichana wapo **milioni 5.64** sawa na **asilimia 50.4**; Kidato cha Tano na Sita, idadi ya wanafunzi wote ni **160,461**,

ambapo wasichana ni **70,370** sawa na **asilimia 43.9**; Vyuo vya Ufundi jumla ya wanafunzi waliopo ni **157,420** ambapo wasichana ni **75,194** sawa na **asilimia 47.8**; na kwa upande wa Vyuo Vikuu idadi ya wanafunzi wote ni **206,167**, wasichana wapo **88,579** sawa na **asilimia 43**. Mafanikio haya yamechangiwa na uamuzi wa Serikali ya Awamu ya Tano kutoa elimu bure kwenye Elimu-msingi na pia kuongeza fedha kwenye Mfuko wa Mikopo wa Elimu ya Juu, ambapo mwaka wa fedha ujao (2021/2022) umetengewa takriban **shilingi bilioni 500** kutoka **shilingi bilioni 464** mwaka za mwaka huu wa fedha (2020/2021).

Hata hivyo, wanawake bado wanakabiliwa na changamoto nyingi katika mifumo ya elimu. Hivi punde tumesikia baadhi ya changamoto, ikiwemo umbali wa

kwenda shuleni, uhaba wa madarasa, mabweni, vyoo, ukosefu wa maji, n.k. Ingawa matatizo hayo yanahusu jinsia zote mbili, lakini ukweli ni kwamba, yanawaathiri zaidi wanawake. Hivyo basi, Serikali itaendelea kujenga miundombinu ya elimu ili kuwaondolea watoto wetu adha hizo. Sambamba na hayo, kwa lengo la kuongeza fursa ya elimu na kuwafanya wanawake wanufaike na maendeleo ya sayansi na teknolojia, mwezi Julai mwaka huu, tutaanza kutekeleza mradi wa kujenga shule moja ya sekondari yenye mabweni, kwenye kila mkoa kwa ajili ya kufundisha masomo ya sayansi kwa wasichana.

***Ndugu Wanawake wenzangu;***

Kuhusu Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi, jitihada kubwa zimefanyika. Tangu tupate Uhuru, Serikali

imeanzisha jumla ya Mifuko 61 ya Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi, ambayo mpaka sasa imetoa mikopo yenye thamani ya **shilingi trilioni 2.22** kwa wanawake **millioni 5.3**. Hata hivyo, hapa inabidi tufanye tathmini ili kujua namna gani fedha hizo zimewanufaisha wanawake.

Sambamba na hayo, mwaka 2018, Serikali ilipitisha Sheria ambayo ilizielekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga **asilimia 10** ya Mapato ya ndani kwa ajili ya kutoa mikopo isiyo na riba (Wanawake 4%, Vijana 4% na Watu wenye Ulemavu 2%). Tangu kipindi hicho, mikopo yenye thamani ya **shilingi bilioni 63.489** imetolewa na kuwanufaisha wanawake **938,802**. Lakini hapa ningependa kutoa wito kwa madiwani kuacha kutumia fedha hizi kujinufaisha kisiasa. Kwenye maeneo mengi fedha za

Mfuko huu zinatolewa kidogo kidogo kama hisani kwa wanawake na hivyo kufanya zishindwe kutimiza malengo yaliyokusudiwa. Na hii ndiyo sababu kwenye maeneo mengi mzunguko na marejesho ya fedha hizi umekuwa mdogo sana. Kwangu mimi, naona ni bora fedha hizo ziwe zinatolewa kiasi kikubwa kidogo kwa vikundi vichache vitakavyoweza kuzitumia na kuzalisha; na kufanya marejesho ya haraka yatakayowezesha ukopeshaji wa vikundi vingine. Hivyo, nawaomba Waheshimiwa Madiwani, hususan wanawake, kuusimamia Mfuko huu kwa mujibu wa sheria ili tuweze kuona matokeo yake. Napenda pia kutumia fursa hii kumwagiza Waziri wa TAMISEMI (ambaye kwa bahati nzuri mwanamke) kushughulikia suala la tuhuma ya upendeleo ya utoaji mikopo ya halmashauri.

Mbali na fedha za halmashauri, Benki ya Posta Tanzania kupitia Dirisha la Wanawake imeendelea kutoa mikopo, ambapo kiasi cha **shilingi bilioni 22.3** kimetolewa kwa wanawake **6,327**. Mtakumbuka kuwa, Serikali katika awamu ya nne ilianzisha Benki ya Wanawake. Hata hivyo, kutokana na uendeshaji usioridhisha, ililazimika kuhamishia shughuli zake kwenye Benki ya Posta, ambayo inajitahidi kufanya vizuri. Kama hali hiyo itaendelea, huko mbeleni, huenda tutaangalia uwezekano wa kuirudisha tena Benki ya Wanawake.

***Ndugu Zangu Wanawake;***

Kuhusu Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi pia, mtakumbuka kuwa, mwaka 2016, wakati nikiwa Makamu wa Rais, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa aliniteua

kuwa Mjumbe wa Jopo la Dunia katika Kumuwezesha Mwanamke Kiuchumi katika nchi za Afrika ya Mashariki na Kusini mwa Jangwa la Sahara. Lengo kuu la Jopo hilo ilikuwa kuandaa mikakati thabiti ya kitaalamu na iliyohakikiwa katika kuziba pengo kati ya wanawake na wanaume duniani kupitia mkakati wa kuwawezesha wanawake kiuchumi. Aidha, kuifanya agenda ya kuwawezesha wanawake kiuchumi kuwa agenda ya kidunia ili kufikia malengo ya maendeleo endelevu ya kufikia usawa wa kijinsia (*SDG 5*).

Katika kutimiza majukumu yangu, kwa hapa nchini, nilibuni wazo la kuanzisha Majukwaa ya Uwezeshaji wa Wanawake kiuchumi. Madhumuni ya Majukwaa hayo ni kuwakutanisha wanawake ili kujadili fursa, changamoto na

jinsi ya kushiriki kikamilifu katika biashara na shughuli nyingine za kiuchumi. Jumla ya majukwaa **23** yameanzishwa katika ngazi ya Mikoa, ambapo nimefarijika kusikia kuwa, mpaka sasa, majukwaa 18 kati ya hayo yanaendelea vizuri. Aidha, kuna majukwaa **144** katika ngazi za Halmashauri za Wilaya, majukwaa **302** katika ngazi ya Kata na majukwaa **522** katika ngazi ya kijiji/mtaa. Majukwaa haya, mbali na kuchochea uanzishwaji wa Vyama ya Ushirika vya Akiba na Mikopo, yamewawezesha wanawake wengi kupata mikopo ya riba nafuu.

Hivyo basi, nitumie fursa hii kuagiza Mikoa, Halmashauri, Kata pamoja na Vijiji au Mitaa kuendelea kuyatunza na kuyasimamia majukwaa haya. Nasisitiza hilo

kwa sababu, nimejipanga kuanza kuyalea na kuyakuza zaidi majukwaa haya kupitia Mfuko wa Rais.

***Ndugu Wanawake;***

Pamoja na jitihada zilizofanyika kwenye uwezeshaji wanawake kiuchumi, changamoto bado zipo. Na moja ya changamoto hizo ni katika umiliki wa mali. Licha ya Sera na Sheria mbalimbali zilizotungwa, kwa sababu mbalimbali, ikiwemo mila na desturi, wanawake wengi hawana uwezo wa kumiliki mali, ikiwemo ardhi na nyumba. Kwa mfano, kwa mujibu wa taarifa zilizopo ni **asilimia 7.4** tu ya wanawake ndiyo wana umiliki wa nyumba wa peke yao ukilinganisha na **asilimia 25.6**. Aidha, wanawake wanaomiliki ardhi ya peke yao wapo **asilimia 8.1** wakati wanaume ni **asilimia 25.0**. Hali hii imekuwa

ikiwakwamisha juhudi za wanawake kujiunua kiuchumi. Kwa hiyo, jitihada za makusudi zinahitajika katika eneo hili, ikiwa ni pamoja na kuihamasisha jamii kuachana na mila na desturi potofu kuhusu wanawake kumiliki mali.

Sambamba na changamoto ya umilikaji mali, wanawake wanakabiliwa na changamoto ya kupata masoko na teknolojia rahisi kwa ajili ya kufanya shughuli zao mbalimbali za kiuchumi. Hivi majuzi nilikutana na viongozi wa sekta binafsi, ambao walinieleza kuhusu changamoto inayowakabili wanawake wengi wajasiriamali wadogo ya kukosa maeneo ya kufanyia shughuli zao. Hii inawalazimisha kufanya shughuli hizo majumbani na hivyo kufanya bidhaa zao zikose ithibati ya ubora na kuwakosesha masoko, hususan ya kimataifa. Napenda

kutumia fursa hii kuahidi kuwa Serikali itaendelea kushughulikia suala hilo pamoja na masuala ya masoko na upatikanaji wa teknolojia rahisi.

***Ndugu Wanawake Wenzangu;***

Eneo jingine ambalo Serikali imefanya jitihada kubwa ni Kutokomeza Vitendo vya Unyanyasaji wa Kijinsia na Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto. Serikali imeanzisha Madawati ya Jinsia na Wanawake katika Vituo vya Polisi **420** ili kuharakisha utoaji wa huduma kwa wahanga. Aidha, jumla ya Kamati **18,186** za Ulinzi na Usalama kwa Wanawake na Watoto zimeanzishwa kwa ajili ya kutoa elimu na huduma kwa jamii kwa wahanga wa ukatili kuanzia ngazi ya Kijiji/Mtaa hadi Taifa. Vilevile, mwaka 2017, Serikali ilitunga Sheria ya Msaada ya Kisheria,

ambayo imewasaidia akina Mama na Watoto wa Kike kupata huduma za Haki zao katika vyombo vya usimamizi wa Sheria. Serikali inaendelea pia kuratibu uanzishwaji wa Madawati ya Jinsia katika Vyuo vya Elimu ya Juu.

Pamoja na hatua hizi, vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia na ukatili dhidi ya wanawake na watoto bado vipo na vinaendelea kuongezeka. Hali hii inatutaka sisi wanawake ambao ni waathirika wakubwa tukae chini tufanye utafiti na kuchekecha vichwa kwa pamoja na wasimamizi wa sheria ili tujue ni wapi tunakwama. Lakini niseme, binafsi naamini kuwa, sisi wanawake tukiamua, tuna uwezo wa kulimaliza tatizo  hili.

*Ndugu Wanawake na Watanzania mnaonisikiliza;*

Kuhusu suala la Kuboresha Huduma za Afya, hususan Afya ya Uzazi, kama mnavyofahamu, tumejitahidi sana kuongeza miundombinu ya kutolea huduma za afya, hususan Hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati. Hii imeenda sambamba na kuongeza idadi ya watumishi wa afya pamoja na upatikanaji dawa, vifaa tiba na vitendanishi, ingawa nakiri kuwa bado tuna pengo kubwa la watumishi.

Hatua hizi zimesaidia kusogeza na kuboresha huduma za afya kwa wananchi, ambapo hivi sasa **asilimia 80** ya watoto wanazaliwa kwenye vituo vya kutolea huduma za afya. Vilevile, nchi yetu ni miongoni mwa zinazoongoza Barani Afrika kwa kutoa chanjo kwa watoto, ambapo tumefikia **asilimia 98**. Hii imesaidia kupunguza vifo vya

akinamama na watoto. Kwa mfano, vifo vya watoto wachanga (*wenye umri chini ya siku 28*) vimepungua hadi **7** kwa kila vizazi hai 1,000; wenye chini ya miaka mitano kwa sasa idadi ya vifo vinavyotokea ni **50** kwa kila vizazi hai 1,000 na vifo vya mama wajawazito imeshuka hadi **321** kwa kila wajawazito 100,000.

Pamoja na mafanikio hayo, idadi ya vifo vinavyotokea kwa wanawake na watoto bado ni kubwa. Hivyo, hatuna budi kuongeza nguvu katika eneo hilo. Sambamba na changamoto hiyo, hivi punde tumeambiwa kuhusu matatizo ya kuendelea kutozwa kwa gharama za huduma ya afya ya mama na mtoto (chanjo, vifaa vya kujifungulia na kulazwa kwa ajili ya kujifungua) pamoja na tatizo la gharama za mgonjwa aliyefariki.

Kuhusu suala la gharama za kujifungua, nataka nirudie maelekezo ya Serikali kuwa huduma hii itolewe bure; na katika hilo nakuagiza Waziri wa Afya (*bahati nzuri ni mwanamke na ni daktari mzoefu*) usimamie suala hilo. Kuhusu gharama za maiti, natoa rai kwa hospitali zote nchini kuweka utaratibu wa kutoa gharama za matibabu mara kwa mara kwa wagonjwa badala ya kusubiri siku ya mwisho. Aidha, endapo mgonjwa atafariki, hospitali hazipaswi kuzuia maiti; badala yake zinapaswa kuruhusu maiti hizo zichukuliwe na kukubaliana na ndugu wa marehemu kuhusu namna ya kulipia gharama zinazodaiwa. Sio utu hata kidogo kuzuia maiti isizikwe au isichukuliwe na ndugu kwa sababu ya deni. Lakini hapa simaanishi kwamba deni lisilipwe.

*Ndugu Wanawake na Watanzania mnaonisikiliza;*
Matatizo mengine yenye kuwasibu wanawake ni upatikanaji wa maji safi na salama, hususan maeneo ya vijijini. Kwa sasa tumefikisha maji kwa wananchi kwa wastani wa **asilimia 74**. Hivyo basi, tumebakisha **asilimia 26**. Tumejipanga, kupitia maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM, kuhakikisha ikifika mwaka 2025, tuwe tumefikisha maji vijijini kwa **asilimia 85** na mijini **asilimia 95** ili hatimaye kufikia lengo la kumtua Mama ndoo kichwani.

Tatizo jingine ni upatikanaji wa umeme vijijini. Tumejipanga hadi ikifika mwaka 2024, tutahakikisha tumefikisha umeme kwenye vijiji vyote. Kazi itakayobaki itakuwa usambazaji. Na hii ndiyo sababu hivi sasa vyuo vyetu vingi vya ufundi vinafundisha vijana wengi fani

mbalimbali za umeme ili wakatusaidie kusambaza umeme vijijini. Na katika hilo, niwaombe wanawake tutumie umeme kiuchumi.

Miundombinu ya usafiri, hususan barabara za vijijini, ni changamoto nyingine inayowahusu wanawake. Awamu mbalimbali za Uongozi wa nchi yetu zilijitahidi kujenga miundombinu ya usafiri na usafirishaji. Lakini nikiri, kasi ya ujenzi wa miundombinu hiyo ilikuwa kubwa zaidi kwenye Awamu iliyopita, Awamu ya Tano. Sisi Awamu ya Sita tumepokea kijiti; na nataka niahidi kuwa tutaendeleza kasi hiyo. Tutakamilisha miradi yote mikubwa ya kimkakati iliyoanzishwa kwenye Awamu ya Tano: barabara, reli ya kisasa, usafiri wa majini, viwanja vya ndege, kikiwemo Kiwanja cha Kimataifa cha Msalato. Zaidi ya hapo,

tutaweka mkazo mkubwa katika kuiwezesha TARURA kifedha na kitaalam ili kuongeza kasi ya ujenzi wa barabara za vijijini, ikiwa ni pamoja na kuangalia suala la teknolojia itakayosaidia barabara hizo kudumu muda mrefu.

Suala la Mazingira ni eneo jingine linalowahusu wanawake. Kwa sasa, katika nchi yetu kuna uharibifu mkubwa wa mazingira, ambapo waathirika wakubwa ni wanawake. Ili kukabiliana na tatizo hili, nawaomba wanawake wenzangu wa Tanzania tukashirikiane katika kutunza mazingira yetu, ikiwemo kufanya usafi kwenye maeneo yetu.

*Ndugu Zangu Wanawake;*

Dunia ya leo inaendeshwa na mifumo ya kidigitali, hata hivyo, kwa hapa nchini, kuna pengo kwenye matumizi ya mifumo hii kwa Wanawake na wanaume. Kwa mujibu wa Taarifa ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 2017, ni **asilimia 61** ya wanawake nchini ndiyo wanatumia huduma rasmi za kifedha wakati wanaume ni **asilimia 71**. Tunafanya jitihada za kupunguza pengo la hilo (*closing the digital gap*) ili kuwezesha wanawake kunufaika na fursa mbalimbali zitokanazo na Mapinduzi ya Nne ya viwanda. Na hii ndiyo moja ya sababu iliyotufanya kuanzisha Mradi wa kujenga shule za sayansi kwa wasichana kila mkoa.

Masuala mengine yenye kuwahusu wanawake ni Sheria na upatikanaji wa Haki pamoja na Utawala Bora. Kuhusu

Sheria na Haki, maboresho makubwa yamefanyika katika eneo hili. Ubora wa majengo ya taasisi katika ngazi zote (Mahakama za Wilaya na za Mwanzo), Mahakama za Kutembea, utunzaji wa Kumbukumbu, ufuatiliaji wa mwenendo wa kesi kwa njia ya kidigitali. Hatua hizi zimeboresha mfumo wa utoaji haki nchini na kuwanufaisha zaidi wanawake.

Kuhusu Utawala Bora, kwa ujumla nchi yetu imepiga hatua kubwa kwenye eneo hili, na hasa katika mapambano dhidi ya rushwa. Tafiti mbalimbali za taasisi za kimataifa zimedhihirisha hilo. Na hapa nataka kuipongeza sana Awamu ya Tano kwa kufanya kazi kubwa katika kupambana na rushwa, ambapo imesaidia kuongeza ufanisi kwenye ofisi za umma. Ninyi ni mashahidi hivi sasa mtu

akienda kwenye taasisi za umma anahudumiwa vizuri. Kwa hiyo, kwa kiasi kikubwa eneo la utawala bora limetusaidia wanawake kutatuliwa matatizo yetu.

***Waheshimiwa Viongozi;***
***Wageni Waalikwa;***
***Ndugu Wanawake wenzangu pamoja***
***na Watanzania mnaonisikiliza;***

Serikali ina dhamira ya dhati ya kuleta usawa wa kijinsia nchini na kuwawezesha wanawake kiuchumi ili kutimiza Azimio Namba 5 la Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG) kuhusu usawa wa jinsia na kuondoa kila aina ya ugandamizaji dhidi ya wanawake na wasichana. Na ili kufikia azma hiyo, masuala ya usawa wa jinsia tumejumuisha kwenye Mpango wetu wa Tatu wa Taifa wa

Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026). Zaidi ya hapo, hivi sasa tunafanya mapitio ya Sera ya Maendeleo ya Jinsia

Lakini, pamoja na azma hiyo nzuri, ni ukweli kuwa, Sera, Sheria, Mipango na jitihada za Serikali peke yake haziwezi kutuhakikishia kutekeleza na kutimiza yote tunayokusudia. Ni lazima tushirikiane na wadau wengine. Hivyo basi, napenda kutumia fursa hii kuyakaribisha mashirika na taasisi za kimataifa, asasi za kiraia, kampuni pamoja na watu binafsi kushirikiana na Serikali ili kuongeza nguvu jitihada za kufikia usawa wa kijinsia na kuwezesha wanawake kiuchumi. Na katika hilo, napenda kuarifu kuwa wakati wa Mkutano wa Afrika – Ufaransa uliofanyika hivi karibuni, nilipewa heshima ya kuchagua eneo moja la

kumjenga mwanamke ili kulisimamia ***(championing)***. Nimeamua kuchagua eneo la Haki za Kiuchumi (*Economic Rights*). Hii inatokana na kutambua kuwa uwezeshaji wanawake kiuchumi ni nguzo muhimu katika kuleta usawa wa kijinisia. Hivyo basi, nawaomba wadau tushirikiane katika hilo. Najua kati yetu hapa wapo vijana wazuri wanaoweza kutoa mchango. Mfano, Mkurugenzi Mtendaji wa NMB na pia Bi. Beng'i Issa, ni miongoni mwa watakaonisaidia.

Lakini, sambamba na kuomba ushirikiano kwa wadau, naihimiza pia jamii nzima kuachana na mtazamo hasi kuhusu wanawake. Wanawake sio viumbe dhaifu; bali ni watu imara na wenye nguvu kama walivyo wanaadamu wengine, na pengine wanawake wana nguvu zaidi. Mama

Eleanor Roosevelt, Mke wa Rais wa zamani wa Marekani, aliwahi kusema, nanukuu *"A woman is like a tea bag, you never know how strong it is until it's in hot water"* akimaanisha kwamba *"Mwanamke ni kama paketi ya majani ya chai, huwezi kuona nguvu yake mpaka iwekwe kwenye maji ya moto"*. Na hii ni kweli kabisa, kwa kutumia mfano wangu mwenyewe. Huko nyuma sikutegemea kama ningeifanya kazi hii lakini sasa naifanya. Na katika hili, najua kwenye jungu hili la maji ya moto siko peke yangu, wanawake wote (mawaziri, wabunge, watendaji wakuu wa taasisi, madiwani, watendaji wa kata na hadi vijiji) ni lazima tushirikiane na kushikamana katika *kukoleza rangi ya majani ya chai* ili kudhihirisha kwamba wanawake tunaweza. Asiwepo mtu mmoja wa kubaki nyuma.

Na hapa natoa rai kwa wanawake wote nchini kujiamini na kujitambua. Ukombozi wa mwanamke unaanza na mwanamke mwenyewe na hiyo ndiyo maana ya kaulimbiu ya Mkutano huu inayosema **"Mwanamke ni Nguzo ya Maendeleo: Tujitambue sisi ni nani, Tujidhatiti kuleta ustawi wa jamii Kiuchumi, Kijamii na Kisiasa, hivyo basi tusimamie na Tutekeleze Wajibu wetu"**. Na katika hilo, nawahimiza wanawake mliobahatika kupata nafasi mbalimbali za uongozi kujitahidi kuwa chachu ili kuhamasisha wanawake wengine wanaotuangalia kama mifano kwao, na hasa wasichana waweze kujiamini na kufika tulipofika sisi. Waingereza wana msemo, *"Litle girls with dreams become woman with vision"* ukiwa na maana kuwa *"Wasichana wenye ndoto ndiyo baadaye hugeuka kuwa wanawake wenye maono"*.

Sambamba na hilo, napenda kutumia fursa hii kuwahasa wanawake wenzangu wengine tunaofanya shughuli mbalimbali, ikiwemo biashara, ujasiriamali, kilimo, n.k.; kujitahidi kuwa wabunifu, na kutengeneza bidhaa zenye ubora pamoja na kutumia fursa zilizopo. Nalisema hili kwa sababu hii nimeeleza kuhusu changamoto ya masoko kwa wanawake, lakini nafahamu ipo Sheria ya Manunuzi inayoelekeza kuwa, **asilimia 30** ya manunuzi ya umma yapewe kwa Makampuni yanayomilikiwa na wanawake. Ukiondoa wanawake kama Sara Masasi, Wazire na wengine wachache). Sina hakika, wanawake wangapi wanaifahamu Sheria hiyo na kuitumia. Hii ndiyo sababu nawahamasisha wanawake wenzangu kuzitafute na kuzitumia fursa.

Mwisho kabisa, na hili nalisema kama mama na mwanamke mwenzenu, kwamba, pamoja na jitihada kubwa tunazozifanya za kutaka usawa wa kijinsia na uwezeshaji kwa jinsia yetu, tusisahau majukumu yetu ya kulea familia na jamii kwa ujumla. Mwanamke ni Mzazi (Mama), Mlezi, Mwalimu, Muuguzi, Msimamizi wa Sheria na Kanuni.

*Baada ya kusema hayo, Mungu atubariki Wanawake wote wa Tanzania na familia zetu.*

*Narudia Kuwasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!*

**"Ahsanteni sana kwa kunisikiliza"**